



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.Kumb.Na.SDC/A20/17/39

Tarehe: 19/07/2021

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Songwe anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya wilaya ya Songwe kuomba nafasi zifuatazo:

1. MTENDAJI WA KIJIJI III -NAFASI TANO (5)

SIFA:

Awe na elimu ya kidato IV au VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii kutoka chuo cha serikali za mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

KAZI NA MAJUKUMU:

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na Msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wanachi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, Umasisikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
- Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea,kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA TGS B

2.DEREVA II-NAFASI MOJA (1)

SIFA

- Cheti cha kidato cha Nne na leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo ameifanyia kazi kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving course) yanayotolewa na chou cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chou kingine kinachotambuliwa na serikali. Waombaji wenyewe cheti cha majoribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

KAZI NA MAJUKUMU

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
 - Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
 - Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
 - Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
 - Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
 - Kufanya usafi wa gari.
 - Kufanya kazi nyingine kadri atakavyo elekezwa na Msimamizi wake.

NGAZI YA MSHAHARA TGS B

MASHARTI YA JUMLA

- A. Mwombaji awe raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka 45
 - B. Barua ya maombi iambatane na wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum vitae).
 - C. Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vivuli vyta vyetini vya kidato cha IV,VI, cheti cha kuzaliwa na vyetini vingine vya taaluma.
 - D. Picha mbili ndogo (Passport size) za hivi karibuni.
 - E. Matokeo ya muda (provision/testimonials/statement of results) havitapokelewa.
 - F. Waombaji wenyewe vyetini vya kidato cha nne na sita waliosoma nje ya nchi

wanatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa NECTA.

G. Waombaji wenyе vyeti vyeti vya Astashahada/ cheti vya nje ya nchi wanatakiwa kuambatanisha uthibitisho wa NACTE.

H. Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.

I. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 1 Agosti,2022.

Barua zote zitumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya wilaya ya Songwe,
S.L.P. 77
Mkwajuni –Songwe

LIMETOLEWA NA:

CPA Cecilia D. Kavishe

Mkurugenzi Mtendaji (W)

SONGWE